
Mada inayofuata: *Kioo na Kivuli*

## SHERIA YA MUNGU
### AMRI KUMI

## SHERIA YA MUSA
### SHERIA YA SHEREHE



# 12a KIOO NA KIVULI



Je, kuna ukinzani katika Biblia? Wala HAKUNA, hata kama yaweza kuonekana hivyo.

Kwa mfano, Yesu Kristo alizungumza kwa kukubaliana ile sheria katika Luka 16:17, na vivyo hivyo ndivyo alivyofanya Mtume Paulo katika Warumi 7:7, 12. Licha ya hili, yaonekana kwamba mtume yule yule anasema kinyume na ile sheria katika Wagalatia 3:10,13. Je, anajipinga mwenyewe?

Pale Mungu alipomwumba mwanadamu, aliweka kanuni za sheria Yake moyoni mwake (Mwanzo 2:16,17). ("usi………").

Mwanadamu, aliyeumbwa akiwa mwenye utashi, aliiasi ile sheria naye akafukuzwa kutoka Edeni (Mwanzo3:24). Mwanadamu alipasa kufa kwa ajili ya dhambi yake, lakini Mungu, kwa rehema Yake, akaweka wa mbadala kwa muda, mwanakondoo, ambaye alikuwa ni mfano wa Kristo, Mwokozi wa wanadamu. Zile ngozi kutoka kwa wale wanyama wa kwanza waliouawa ziliwapatia wanadamu mavazi (Mwanzo 3:21).

Kafara ya Habili ilikubaliwa. Alitoa mwana kondoo, ambapo kaka yake alileta matunda ya nchi naye akakataliwa na Mungu (Mwanzo 4:3, 4). Ili kusamehewa, mwenye dhambi alipaswa kuleta mnyama hekaluni, akaweka mikono yake juu ya kichwa cha yule mnyama, na kumtoa kafara. Hii iliashiria kwamba dhambi zake zilihamishiwa kwa yule mnyama, ambaye alikufa mahali pake (Walawi 4:27-29). Desturi hizi zote pamoja na maadhimisho, yalikuwa ni kivuli ama mfano ulioelekeza kwa Kristo. Kwa sababu hii, inaitwa kuwa ni Sheria ya Maadhimisho (Waebrania 10:1).

**1. Kuna aina ngapi za sheria?**

*Kando ya sheria za kijamii katika Israeli, Biblia inaeleza juu ya sheria nyingine mbili:*

a) Amri Kumi, ambazo zaweza kulinganishwa na kioo kinachotuonesha sisi juu ya hali yetu ya dhambi.

b) Sheria ya maadhimisho, ambayo inajumuisha pamoja na kafara, maadhimisho na sikukuu, ambazo zilikuwa ni kivuli ama mfano wa Kristo pamoja na kazi yake kwa mwanadamu.

Sheria hii alipewa mwanadamu baada ya anguko lake nayo ilikuwa ni njia ya ukombozi wake hata pale Mwana wa Mungu alipokuja na kufa katika dunia hii, mahali petu.

*Sheria hii alipewa mwanadamu baada ya anguko lake nayo ilikuwa ni njia ya ukombozi wake hata pale Mwana wa Mungu alipokuja na kufa katika dunia hii, mahali petu.*

**2. Je, kuna tofauti zipi kati ya sheria hizi mbili?**

*Katika jedwali ukurasa ufuatao, tutazilinganisha sheria hizo mbili (iangalie hivi sasa).*

**3. Je, ni kwa nini zile Amri Kumi hazikubatilishwa baada ya kifo cha Kristo?**

*Katika Agano la Kale na Agano Jipya, kile kioo cha sheria takatifu ya Mungu ilikuwa ni muhimu ili kwamba mwanadamu aweze kuitambua dhambi. Kilichobadili ilikuwa ni njia ambavyo msamaha ulivyopatikana. Katika Agano la Kale, mwana kondoo, ambaye alichukua mahali mwenye dhambi na kuelekeza mbele kwa Kristo, alipasa kutolewa kafara, ambapo katika Agano Jipya, pale tunapoziona dhambi zetu kulingana na ile sheria, tunaenda moja kwa moja kwa Kristo kwa njia ya imani. Pale Mwokozi alipokuja, ile sheria ya maadhimisho iliyomwakilisha Yeye haikuwa tena na umuhimu.*

**4. Je, Paulo anasemaje juu ya kutahiriwa? Je, hii nayo ilikuwa ni sehemu ya ile sheria ya maadhimisho? 1 Wakorintho 7:19.**

________________________________________________________

Elimu inatuambia ya kwamba kuna faida pale tunapoishi kwa kulingana na mpango wa maadili ya milele, kwani ahadi za Mungu ni kwa ajili ya wale wanaoishika sheria Yake. Kumbukumbu 5:29; Zaburi 119:165.

| *AMRI KUMI* | *SHERIA YA MAADHIMISHO* |
|---|---|
| **1. Zinaitwa kama SHERIA YA MUNGU (Warumi 7:22)** | **1. Inaitwa kama sheria ya Musa (Matendo 15:5).** |
| **2. Ilitolewa tokea Edeni (Warumi 2:15)** | **2. Ilitolewa baada ya Edeni (Wagalatia 3:19)** |
| **3. Iliandikwa kwa chanda cha Mungu (Kutoka 31:18).** | **3. Iliandikwa na Musa (Kumbukumbu 31:24).** |
| **4. Ziliandikwa juu ya mawe (kitu imara).** | **4. Ni kitabu.** |
| **5. Ziliwekwa ndani ya Sanduku la Agano, mahali patakatifu zaidi, ambayo ni ishara ya kiti cha enzi cha Mungu (Kumbukumbu 10:1-5).** | **5. Iliwekwa kando ya Sanduku la Agano (Kumbukumbu 31:25, 26).** |
| **6. Sheria inafananishwa na kioo; inatuonesha hali yetu ya dhambi (Warumi 7:7).** | **6. Sheria ya maadhimisho ilikuwa kwa ajili ya upatanisho ama msamaha wa dhambi (Waebrania 9:22).** |
| **7. Ilikuwa ni njia ya maisha ambayo tunapasa Kuishi kwa hiyo (1 Timotheo 1:8-10).** | **7. Ilikuwa tu ni ishara inayotuelekeza kwa Kristo (Waebrania 9:9).** |
| **8. Ni za milele, Kristo hakuzibatilisha (Zaburi 111:7, 8; Mathayo 5:17).** | **8. Ilibatilishwa na Kristo (Wakolosai 2:14).** |
| **9. Unabii ulisema ya kwamba Yesu angeiadhimisha sheria (Isaya 42:21).** | **9. Paulo asema wazi ya kwamba Yesu aliibatilisha sheria ya maadhimisho (Waefeso 2:15).** |
| **10. Yule anayeishika sheria ya Mungu anaitwa kuwa aliyebarikiwa (Yakobo 1:25).** | **10. Yule anayeyashika yale yaliyoandikwa katika kitabu cha sheria anaitwa kuwa aliyelaaniwa. Baada ya kifo cha Kristo, hapana haja ya desturi hizi (Wagalatia 3:10-13).** |
| **11. Tutahukumiwa kwa sheria (Yakobo 2:10-12).** | **11. Tusihukumiwe kwa kile tulacho, tunywacho, Sikukuu (Sabato za maadhimisho n.k.) ambazo zilikuwa ni kivuli cha yale yatakayokuja (Wagalatia 2:16, 17).** |
| **12. Twaweza kuzishika zile Amri Kumi kwa msaada wa Mungu (1 Yohana 5:3).** | **12. Sheria ya Musa haikuwezekana kuishika (Matendo 15:10).** |

***Uamuzi wangu:*** *Ninakubali ya kwamba zile Amri Kumi, sheria ya Mungu; na ile sheria ya Musa, ambayo ni sheria ya maadhimisho, ni sheria mbili zilizo tofauti. Ile ya kwanza ni ya milele na ile ya pili ni ya kitambo.* ○ *Ndio* ○ *Hapana*